**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MJI HANDENI**

**SHULE YA SEKONDARI HANDENI**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU– TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MJI HANDENI**

**SHULE YA SEKONDARI HANDENI**

**S. L. P. 271,**

**HANDENI.**

**Tarehe ……………**

**<u>NAMBA ZA SIMU</u>:**

Mkuu wa Shule: 0717018235/0757094277

Makamu mkuu wa shule: 0713868570

Patron: 0788042114

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI HANDENI HALMASHAURI YA MJI HANDENI MKOA WA TANGA MWAKA………………………………**

Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano mwaka 2025/2026 katika tahasusi ya……… Shule ya Sekondari ya Handeni ipo umbali wa Kilometa 1 upande mashariki kutoka ofisi ya Halmashauri ya Mji Handeni. Usafiri wa pikipiki kutoka standi kuu ya Handeni unapatikana na ni shilingi 1000/= tu mpaka Shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **..................................** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **.........................** Mwisho wa kuripoti ni tarehe

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**
**2.1. SARE ZA SHULE.**

a. Suruali 2: - Rangi ya bluu nyeusi (dark blue) yenye marinda mawili kila upande isiwe inabana (upana chini iwe inchi 15) kwa ajili ya darasani na suruali 2 rangi nyeusi kwa ajili ya shughuli za nje.
b. Shati 2**:** - nyeupe mikono mifupi lisilobana na lisiwe fupi ili aweze kuchomekea kwa urahisi.
c. Sweta**: -** Kijani kibichi, V-shape (inapatikana duka la shule) na linavaliwa kipindi cha baridi tu. **Majaketi na makoti hayaruhusiwi kabisa**.

**N: B. NGUO ZA NYUMBANI NA SIMU HAVIRUHUSIWI KABISA SHULENI.**

d. Viatu: Vyeusi vyenye kamba na visiwe na kisigino kirefu wala shingo ndefu wala vilivyochongoka, Socks ni nyeusi.
e. Mkanda- Mweusi usiwe na bakozi kubwa na uwe na upana usiozidi inchi 11/2 au sentimita 31/2
f. Fulana 2 rangi ya kijivu za sare ya shule (zinapatikana duka la shule)
g. Nguo za michezo – Traki suti ya kijivu au blue (zinapatikana duka la shule), raba za michezo aje nazo.

**2.3 VYOMBO VYA CHAKULA.**

a. sahani na bakuli
b. kijiko
c. kikombe

***N.B. SHULE HAINA HUDUMA YA CHAKULA MAALUMU. (SPECIAL DIET).***

### 2.4 MAHITAJI MENGINE

Mwanafunzi aje na vifaa vya kujifunzia kama ifuatavyo:

a. Daftari zisizopungua kumi (10)
b. Kalamu za kutosha.
c. Mkebe wa mahesabu (Mathematical set)
d. Ndoo ndogo 1 na kubwa 1
e. Jembe 1, kwanja 1, fagio 1 la chelewa na Brashi 1 ya kudekia (squeezer)
f. Rimu ya karatasi nyeupe A4 mbili (2) na Ruled paper rimu 1 na vitabu vya mchepuo wake (ORODHA YA VITABU IMEAMBATANISHWA NA FOMU HII)
g. Dissecting kit kwa wanafunzi wa somo la Biolojia tu. (**ITAKAGULIWA**)
h. Scientific calculator kwa wanafunzi wa tahasusi za **CBG** na **PCB (ITAKAGULIWA)**
i. Stop watch kwa wanafunzi wa tahasusi za CBG na PCB (**ITAKAGULIWA**)
j. sanduku la bati(trunker) na kufuli.
k. ufagio 1 wa ndani brashi laini (soft bloom) kwa tahasusi ya PCB na HGFa
l. Ufagio 1 wa brushi ngumu (hard bloom) kwa tahasusi ya CBG
m. Brashi za chooni 2 (toilet brush) kwa tahasusi si HGK
n. Reki 1 kwa tahasusi ya HGL
o. Panga 1 kwa tahasusi ya HGLi

2.5 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

*Fedha yote ilipwe **NMB** akaunti namba **41401200062.** (Jina la akaunti **HANDENI SECONDARY SCHOOL**)*

Mwanafunzi aje na nakala halisi ya malipo ya benki (bank pay slip) ikiwa imeandikwa jina halisi la mwanafunzi. (**HATUPOKEA FEDHA MKONONI**)

***MUHUMU:***

- ***TUNAOMBA MICHANGO IANZE KUINGIZWA KUANZIA TAREHE 01/07/2025.***
- ***MWANAFUNZI AJE NA NAKALA YA RESULT SLIP YAKE YA KIDATO CHA NNE NA NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA.***
- ***MZAZI/MLEZI HAKIKISHA MWANAO ANAKUWA NA BIMA YA AFYA. 10,000/= BIMA YA CHF***

## 3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
c. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
i. Kutunza mali za shule;
j. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
k. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***KARIBU SANA HANDENI SEKONDARI***

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………….**

**Jina la Mkuu wa Shule: LUSUBILO SADOCK SICHONE**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI**

***UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO*: -**

- **Mkuu wa shule: 0717018235/0757094277**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0713868570**
- **Mwandamizi Taaluma: 0717916169**
- **Mwandamizi Malezi: 0655833137**
- **Mwalimu wa Duka:0620613654 (Piga kwa msaada vifaa vya dukani**

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**LOCAL GOVERNMENT AND REGIONAL ADMINSTRATION**
**HANDENI TOWN COUNCIL**

(A): REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

HANDENI SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 271,
**HANDENI.**
Tarehe………………………….

MEDICAL OFFICER, …………………..
GOVN.HOSPITAL………………………………………..
……………………………………….

**NAME OF PUPIL……………………………………………………………………………………………………………………..**
Please examine the above-named student to ascertain her fitness for further studies.

**……………………..**
**HEADMASTER**

**MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by the medical officer)
I have examined the above named student with regard to:
Skin……………………………………………………………………………………………………
Eyes……………………………………………………………………………………………………
Ears……………………………………………………………………………………………………
Chest…………………………………………………………………………………………………
Spleen…………………………………………………………………………………………………
Abdomen………………………………………………………………………………………………
Urine…………………………………………………………………………………………………
Stool……………………………………………………………………………………………
Hemoglobin……………………………………………………………………………………………

And I considered:
He is good health, free from infection diseases, worms, bilharzias and fit to go to school.
He is now fit to return to school having treatment
for……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

**………………………………………………………………………………**  **…………………………….**
**NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER**  **DATE**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI – HANDENI**

HANDENI SEKONDARI
S. L. P. 271,
**HANDENI.**

Tarehe ……………………….

**(B&C): FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA**

**SEHEMU A**: Habari za Mwanafunzi.
Jina kamil………………………………………………………………………………………………………
Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………………………………………….
Wilaya alipozaliwa………………………………………………………Kijiji ………………………………………………

**Kukubali nafasi (Ijazwe na mwanafunzi)**
Mimi ………………………………………… nimeona maagizo yote ya kujiunga na shule ya Sekondari ya Handeni na ninakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule. Nitakapokuwa shuleni Handeni sekondari nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata Elimu ya kujitegemea.

Sahihi ya Mwanafunzi……………………….        Tarehe………………………..

**SEHEMU B:** Habari za Mzazi/Mlezi (Ijazwe na Mzazi/Mlezi)
Jina kamili…………………………………………………………………………………………………………
Yeye ni Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………………………………
Kazi yake ……………………………………………………………………………………………………
Anwani ya Mzazi/Mlezi
……………………………………………………………………
……………………………………………………………………
Namba tatu za simu ikiwemo ya Mzazi/Mlezi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi
(a)…………………………………………………………………………………………………………………………………
(b)…………………………………………………………………………………………………………………………………
(c)………………………………………………………………………………………………………………………………..

**UTHIBITISHO**
Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………….. nimehakikisha kwamba maagizo yote yemeeleweka na mtoto wangu amejaza kikamilifu sehemu A. Pia nitahakikisha mtoto wangu anafuata na kutii sheria, kanuni na taratibu zote za shule.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi………………………..        Tarehe…………………

## NJOO NA VITABU VYA TAHASUSI (COMBINATION) YAKO MUHIMU SANA

### HISTORY

1. Mastering History by Carto (pp 1 & 2)
2. S. Yassin (2010) Essential in Advanced Level History (paper 1&2)

### GEOGRAPHY

1. Human and Economic Geography by Goh Ching Leong & Gillian C Morgan (2nd Edition)
2. Certificate Physical and Human Geography by Goh Ching Leong (3rd Edition)
3. Principle of Physical Geography by F. Monk house (2000)
4. Practical Geography of Africa by Prichard j, M. (1976)

### ENGLISH LANGUAGE

**(a) LANGUAGE II BOOKS**

**PLAYS**

1. Betrayal in the City by Francis Ndunguru
2. I Will Marry When I Want by Ngugi Wa Thiong'o
3. An Enemy of the People by Henrik Ibson
4. Black Mamba by John Ruganda

**NOVELS AND SHORT STORIES**

1. The Beautiful One Are Not Yet Born by Ayi Kwei Armah
2. A Man Of The People by Chinua Achebe
3. Divine Providence by Severin N. Ndunguru
4. His Excellency The Head Of The State by Danny Safo

**POETRY**

1. Selected Poem by Institute Of Education
2. The Wonderful Surgeon and Other Poems by Charles Mloka
3. Literature Theory and Analysis by Nicholaus Asheli (3rd Edition)

**(b) LANGUAGE I BOOKS**

1. Advanced level, English Language A practical Approach 4th Edition by Nicholaus Asheli
2. English language I by Oxford

**KISWAHILI –**

**(a) Riwaya:**
Vuta ni kuvute, Usiku utakapokwisha, Mfadhili na Kufikirika.

**(b) Ushairi:**
Kimbunga, Chungu Tamu, Fungate ya Uhuru na Mapenzi Bora

**(c) Tamthilia:**
Nguzo mama, Kwenye ukingo wa thim, Morani na Kivuli kinaishi

**GENERAL STUDIES** - (a) A level General studies Notes

**CHEMISTRY**

1. General Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Five and Six (TIE)
2. Physical Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Five and Six (TIE)
3. Organic Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Five and Six (TIE)
4. Inorganic Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Five and Six (TIE)

**BIOLOGY**

1. Biology Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Five (TIE)
2. Biology Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Six (TIE)

**PHYSICS**

1. Principles of Physics Chand (1&2)
2. Nelkon and Park ($7^{th}$ Edition)

***BASIC APPLIED MATHEMATICS***

Basic Applied Mathematics Form five and six by TIE (2019)

**N. B. VITABU HIVYO NI MALI YA MWANAFUNZI**